# Uamilifu wa Mkazo katika Kiswahili Sanifu

Faraja J. Mwendamseke


## Ikisiri

Mkazo ni hali ya neno au silabi katika neno kusikika kwa nguvu au kuwa na nguvu zaidi kuliko maneno au silabi nyingine (taz. Crystal, 1987:288; Massamba, 2004:52; Kihore, Massamba na Msanjila, 2008:28). Makala hii inahusu uamilifu wa mkazo katika Kiswahili sanifu. Kumekuwapo na mkanganyiko wa uamilifu wa kipambasauti[1] mkazo na vipambasauti vingine ambavyo ni kiimbo na kidatu katika Kiswahili sanifu. Mgullu (1996) anaelezea uamilifu wa mkazo juujuu lakini katika uelezaji wake anachanganya na uamilifu wa kiimbo. Hivyo makala hii imechunguza uamilifu wa mkazo katika Kiswahili sanifu ili kuondoa mkanganyiko huo. Tunapozungumza uamilifu wa mkazo tunarejelea dhima za mkazo. Uamilifu wa mkazo unajitokeza katika kiwango cha tungo neno na kiwango cha tungo kirai na sentensi. Hivyo, makala hii imeweza kubaini kuwa mkazo katika kiwango cha tungo neno na tungo kirai na sentensi kwa kawaida huwa na uamilifu wa kuwekewa nguvu katika silabi au neno wakati wa utamkaji. Ambapo huonesha msigano wa msikiko katika viambajengo vinavyohusika. Aidha, kuna wakati mkazo huwa na uamilifu wa kuonesha msisitizo katika kiambajengo kinachohusika yaani katika tungo neno au tungo kirai na sentensi. Hata hivyo, katika kiwango cha tungo neno ni mara chache sana mkazo unapohama husababisha maana ya msingi ya neno kubadilika. Hivyo, uamilifu wa mkazo umesaidia kubaini kuwa kipambasauti mkazo kina uamilifu tofauti na kipambasauti kiimbo na kidatu katika Kiswahili sanifu. Aidha, kuna mazingira mengine kiimbo na kidatu huweza kuathiri mkazo lakini licha ya athari hiyo ya kimsikiko haibadili uamilifu wa mkazo.


## 1.0 Utangulizi

Dhana ya mkazo imefasiliwa na waandishi kadhaa, kama ifuatavyo; Hogg na McCully (1987:28) wanaona mkazo ni kipandesauti huru cha irabu ambacho kinawakilishwa na seti za sheria. Crystal (1987:288) anasema kuwa mkazo ni kiwango cha nguvu kinachotumiwa kutamka silabi; nguvu hiyo huweza kutofautisha silabi zenye mkazo ambazo hutamkwa kwa nguvu zaidi na silabi zisizokuwa na mkazo ambazo hazitamkwi kwa nguvu sana. Massamba (2004:52) anasema mkazo ni hali ya neno au silabi katika neno kusikika kuwa na nguvu zaidi kuliko maneno au silabi nyingine. Kihore na wenzake (2008:28) wanasema mkazo ni utaratibu wa utamkaji wa maneno ambapo silabi fulani hutamkwa kwa nguvu nyingi zaidi kuliko ilivyo katika silabi nyingine za neno hilohilo. Kutokana na fasili hizo, katika makala hii tunajikita katika fasili za Crystal (1987), Massamba (2004) na Kihore na wenzake (2008) kwa sababu zinaonesha wazi kabisa kuwa mkazo ni hali ya neno au silabi katika neno kusikika kwa nguvu au kuwa na nguvu zaidi kuliko maneno au silabi nyingine. Hivyo, katika makala hii tunapozungumzia mkazo tunamaanisha fasili hii.

Lugha mbalimbali zinaweza kuwa na namna tofauti tofauti za mkazo katika kiwango cha neno, maneno ambatani, kirai na sentensi (Halle & Clements, 1983:15-17; Hogg & McCully, 1987:1-5; Massamba, 2011:211-219). Mkazo ni kipambasauti ambacho

---

[1] Kipambasauti ni kipengele ambacho huhusishwa na vitamkwa vijengavyo maneno katika utamkaji wake. Hubainika tu kinapokuwa kimehusishwa na kitamkwa; hakiwezi kusimama peke yake bila kuhusishwa na kitamkwa (taz. Massamba, 2011:24-25).

hujidhihirisha katika lugha mbalimbali kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kiswahili. Kwa hiyo, mkazo ni sifa muhimu sana katika lugha hizi, ambapo silabi au neno lenye mkazo hutamkwa kwa nguvu zaidi kuliko silabi au maneno mengine. Mkazo katika lugha ya Kiingereza angalau umefanyiwa utafiti wa kina zaidi (taz. Chomsky & Halle 1968:59-145; Liberman & Prince 1977 na Hogg & McCully 1987). Kihore na wenzake (2008:28) wanaeleza kuwa ni muhimu kuzingatia kwamba baadhi ya lugha hazitumii mkazo kama mojawapo ya sifa zake kuu, kwa mfano lugha nyingi za Kibantu hutumia zaidi toni kuliko mkazo. Hivyo, katika baadhi ya lugha za Kibantu kuna lugha chache tu zenye mkazo. Kwa mfano, Philipson (1994) anataja lugha zenye mkazo kama vile Kiswahili, Kikutu na Kizaramo (taz. Massamba 2002). Hii ina maana kwamba kiasilia lugha zote za Kibantu katika kipindi cha Mame-Bantu zilikuwa na toni lakini mabadiliko ya baadaye kabisa yaliyotokea katika baadhi ya lugha hizo yakasababisha sifa ya toni katika baadhi ya lugha kupotea na badala yake zikawa na sifa ya mkazo.

Mkazo katika Kiswahili sanifu umewahi kuelezwa na baadhi ya wataalamu kama vile Halle na Clements (1983:16), Mgullu (1999:79), Kihore na wenzake (2008:28-30) na Massamba (2011:203-241) ambao wanadokeza tu kuwa Kiswahili sanifu kina mkazo. Clements (1983) na Kihore na wenzake (2008) wanaeleza mkazo katika kiwango cha neno ambapo wanaeleza kuwa mkazo huangukia katika silabi ya mwisho kasa moja katika neno. Katika tafiti hizo mkazo msingi tu ndio umebainishwa. Massamba (2011:218) anaeleza zaidi kuwa katika Kiswahili sanifu, katika kiwango cha kirai mkazo unahamia katika neno la mwisho. Tafiti hizi zinadhihirisha kuwa Kiswahili sanifu ina mkazo. Kutokana na umuhimu wa kipambasauti mkazo katika Kiswahili sanifu, kuna haja ya kuchunguza uamilifu wake. Uamilifu wa mkazo unasaidia kukamilisha uzungumzaji katika utamkaji wa viambajengo vinavyohusika. Pia unasaidia kutofautisha kipambasauti mkazo na vipambasauti vingine kama vile kiimbo na kidatu katika Kiswahili sanifu. Hivyo makala hii imechunguza uamilifu wa mkazo katika Kiswahili sanifu.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Ili tuchunguze uamilifu wa mkazo katika Kiswahili sanifu hatuna budi kutumia kiunzi cha Nadharia ya Fonolojia Mizani (kuanzia sasa FM). FM ni kiunzi cha nadharia kilichopendekezwa na Liberman (1975) katika tasnifu yake ya uzamivu ya "The Intonation System of English". Kiunzi hiki kilipendekezwa kwa sababu ya kujaribu kutatua matatizo yaliyokuwa yakijitokeza katika uchanganuzi wa mkazo katika lugha ya Kiingereza kwa kutumia Kiunzi Rasmi cha Fonolojia Zalishi (kuanzia sasa KRFZ). Hivyo aliachana na fikra kwamba mkazo ulikuwa sifa ya vipandesauti maalumu bali mkazo ni kipambasauti ambacho kinapaswa kuchukuliwa kuwa kinajitegemea. Kiunzi cha FM baadaye kikaendelezwa na Liberman na Prince (1977) na kufafanuliwa zaidi na Halle na Vergnaud (1978).

Nadharia ya FM imeegemezwa kwenye misingi mikuu mitatu, nayo ni: mosi, silabi[2] kama kiambajengo muhimu, maneno ya lugha hupangika katika utaratibu wa silabi unaofuata mpangilio wa lugha maalumu inayohusika. Hivyo, kiuchanganuzi silabi zina umuhimu mkubwa kwa sababu mkazo huwekwa kwenye kilele cha silabi. Pili, umuhimu wa nguvumsikiko, katika nadharia ya FM, uchanganuzi wa sauti umekitwa katika kigezo cha nguvumsikiko ili kutofautisha silabi zenye msikiko mkubwa dhidi ya silabi zisizo na msikiko mkubwa, na kupambanua mpandoshuko wa mawimbi ya sauti wakati wa usemaji. Aidha, husaidia kujua silabi huanzia wapi na kuishia wapi. Tatu, uhusiano wa ndani wa silabi, uhusiano huu huoneshwa kwa kutumia matawi ya mizani, Liberman na Prince (1977) walisisitiza kuonesha uhusiano wa ndani wa silabi mbalimbali zilizomo katika neno au kirai.

Nadharia ya FM ina mihimili mitatu, ambayo hubeba dhana ya nguvu na uhafifu. Mosi, ni mpangilio msonge. Hapa vipengele vya kifonolojia huwakilishwa **katika** rusu zilizo **katika** uhusiano wa kimsonge, kwa kuanza na vipengele vipana zaidi kisha kumalizia na vipengele vidogo zaidi (taz. Massamba, 2011:208). Pili, matumizi ya matawi. Haya yanakuwa katika jozi zenye uwilikinzani. Matawi haya huanzia sehemu moja katika uwili wake na kila moja likaishia sehemu yake. Matawi haya hutofautiana na miti ya kisintaksia kwa sababu katika miti ya sintaksia kuna uwezekano wa kuwa na matawi matatu wakati mwingine. Katika FM kila mwisho wa tawi huitwa kikonyo. Matawi yanayoanzia katika kikonyo kimoja huweza kuishia katika vikonyo viwili. Vikonyo hivyo viwili hujulikana kama vikonyo dada. Kumbuka tunapochora miti ya mizani kadhaa kama walivyopendekeza Liberman na Prince huwa tunaanza na K (kiini) (wao walitumia R (Root) kwa sababu walikuwa wanashughulikia lugha ya Kiingereza). Hivyo hiki ni kikonyo cha juu kabisa, lakini kikonyo hiki si lazima kila mara kionyeshwe.

Tatu, uhusiano wiani wa matawi, hii hujidhihirisha pale ambapo huwa na uwiani wa kimsikiko. Hivyo tawi moja huwa na msikiko zaidi kuliko tawi jingine. Tawi lenye msikiko zaidi huwa na nguvu zaidi na hupewa alama ya N; alama hii inasomeka “ina **n**guvu zaidi kuliko…” wakati lile lisilo na msikiko zaidi huwa hafifu na hupewa alama ya H; alama hii inasomeka “ni **h**afifu kuliko…” (taz. Liberman na Prince, 1977: 257; Massamba, 2011: 209).

Hivyo ili kutimiza malengo ya makala hii, nadharia ya FM imetumika ili kuonesha kwa uwazi msigano wa msikiko wa viambajengo vinavyohusika. Pia, uhamaji wa mkazo, ambao utabainisha namna mkazo unavyoweza kuhama kutoka silabi moja hadi nyingine katika neno au kutoka neno moja hadi lingine katika kirai au sentensi. Hii imesaidia kubaini uamilifu wa mkazo katika Kiswahili sanifu.

---

[2] Massamba (2004) anafasili silabi kuwa ni dhana ya kifonolojia katika utamkaji wa maneno ambayo inawakilisha umbo la kimatamshi ambapo sauti moja au zaidi hutamkwa kwa mara moja kama fungu moja.


**3.0 Uamilifu wa Mkazo**

Mkazo ni mojawapo wa kipambasauti ambacho kina uamilifu katika lugha inayohusika. Hivyo tunapozungumzia uamilifu wa mkazo ni kwamba tunarejelea dhima ya mkazo katika lugha. Yaani kipambasauti hiki kinapojibainisha katika tungo neno au tungo kirai na sentensi huwa kina dhima gani? Uamilifu wa mkazo unachunguzwa kwa kuangalia mkazo unavyojibainisha katika viambajengo vinavyohusika. Pia, pale mkazo msingi[3] unapohama kutoka kiambajengo kimoja hadi kiambajengo kingine kutokana na michakato ya kifonolojia, kimofolojia ama kisintaksia (taz. Hogg na McCully, 1987). Hivyo uamilifu wa mkazo hujibainisha katika kiwango cha tungo neno na kiwango cha tungo kirai na sentensi.

**3.1 Uamilifu wa Mkazo katika Kiwango cha Tungo Neno**

Katika Kiswahili sanifu uamilifu wa mkazo katika kiwango cha tungo neno unajitokeza katika namna tofauti tofauti. Kwanza, uamilifu wa mkazo ni kuwekewa nguvu kwenye silabi wakati wa utamkaji ambapo husaidia kutofautisha kiwango cha nguvu ya msikiko kati ya kipandesauti kimoja na kipandesauti kingine. Hii hutofautisha silabi yenye msikiko mkubwa zaidi kuliko silabi nyingine katika neno hilo. Dhima hii inajitokeza kwa kiasi kikubwa katika Kiswahili sanifu. Hatahivyo, licha ya mkazo kutofautisha msikiko wa sauti lakini kwa kawaida mkazo msingi katika kiwango cha neno huangukia silabi ya pili kutoka mwisho (taz. Halle na Clements, 1983: 17- 18; Massamba, 2011: 218-225). Hii inadhihirisha wazi kabisa kipambasauti mkazo katika Kiswahili sanifu ni sifa muhimu sana ya kiarudhi[4] ili kuweza kutamka maneno sawasawa. Hii ndio inadhihirisha hali ya usemaji wa kawaida katika Kiswahili sanifu. Hivyo inalingana na lugha zinazotumia mkazo kama vile lugha ya Kiingereza na Kifaransa ambapo mkazo katika kiwango cha tungo neno hutofautisha msigano wa msikiko miongoni mwa silabi katika neno. Tazama mfano namba 1, ufuataο:

1 Mama




= ma`ma

Ufunguo: K: Kiini N: Nguvu H: Hafifu

Mfano namba 1 hapo juu unaonesha wazi kabisa mkazo unatofautisha msikiko wa sauti miongoni mwa silabi zinazounda neno linalohusika. Neno "*mama*" lina silabi mbili lakini silabi hizi zimetamkwa kwa kuwekewa nguvu ya msikiko lakini kiwango cha

[3] Pale kiambajengo kinapotamkwa hutamkwa kwa nguvu zaidi kuliko viambajengo vingine.

[4] Ni kijenzi cha sauti ambacho chenyewe ni huru lakini hupata vikahusishwa na vitamkwa katika usemaji ili kujenga usemi unaokidhi katika mawasiliano

nguvu kinatofautiana. Yaani silabi **ma** ya pili kasa moja hutamkwa kwa nguvu zaidi kuliko silabi **ma** ya mwisho katika neno hilo yaani ni hafifu kimsikiko.

Pili, mkazo unaweza ukaonesha msisitizo wa jambo. Hii hujitokeza zaidi katika maneno ambayo yanatokana na mchakato wa kimofolojia ambao ni uradidi. Hivyo ili kuonesha msisitizo wa jambo mkazo msingi unahamishiwa katika silabi ya kwanza ya neno kutoka katika silabi ya mwisho kasa moja. Hata hivyo, licha ya uhamaji wa mkazo kutoka silabi moja kwenda silabi nyingine, maneno hayo hayajaweza kubadili maana ya msingi ya neno linalohusika. Hii inadhihirisha kuwa kiasilia mkazo hauwezi kubadili maana ya msingi ya kileksika au kisarufi (taz. Liberman na Prince, 1977; Kager, 1996 na Massamba, 2011). Mfano namba 2 (a-d) unaonesha namna uhamaji wa mkazo unavyoonesha msisitizo katika neno linalohusika.

2 (a) Hapaha`pa linganisha na ha`pahapa
(b) Kuleku`le linganisha na ku`lekule
(c) Vilevi`le linganisha na vi`levile
(d) Hukuhu`ku linganisha na hu`kuhuku

Mifano iliyopo katika 2 (a-d) inaonesha dhahiri kuwa uhamaji wa mkazo msingi katika Kiswahili sanifu haujaweza kubadili maana ya msingi ya neno. Uhamaji huo umeonesha msisitizo katika maneno hayo. Hata hivyo, katika Kiswahili sanifu uradidi hutokea hasa katika viwakilishi vioneshi. Kwa upande wa lugha ya Kiingereza, mara nyingi mkazo unapohama kutoka silabi moja kwenda nyingine katika neno mkazo hubadili kategoria ya neno. Hebu tuone mifano ifuatayo iliyotolewa katika Massamba (2012: 164):

3 (a) `compound (n): eneo lililozungushiwa uzio ambamo ndani mwake mna nyumba au kiwanja cha kuchezea au kiwanda.
(b) com`pound (kt): fanya kuwa mbaya zaidi au kubwa zaidi.

Mfano 3 (a-b) unadhihirisha kuwa mkazo msingi unapokuwa kwenye silabi ya kwanza neno linakuwa katika kategoria ya nomino. Aidha, mkazo msingi unapokuwa katika silabi ya pili kategoria ya neno hubadilika na kuwa kitenzi. Licha ya kubadilika kwa kategoria ya neno, vilevile maana ya msingi ya maneno hayo imebadilika kabisa. Hali hii inadhihirisha wazi kuwa mkazo katika lugha ya Kiingereza hutumika kutofautisha maana ya maneno yanayohusika (taz. Halle na Clements, 1983).

Katika Kiswahili sanifu, baadhi ya maneno yenye maumbo sawa lakini maana tofauti huweza kutofautishwa kwa kutumia mkazo. Aidha, uamilifu huu hujitokeza mara chache sana katika Kiswahili sanifu. Mifano namba 4 (a- d) inadhihirisha dhima hiyo:

4 (a) (i) baraba`ra (njia kuu)

(ii) bara`bara (sawasawa)
(b) (i) kataka`ta (fanya vipande vipande)
(ii) kata`kata (kabisa kabisa)
(c) (i) hivihi`vi (bila sababu)
(ii) hivi`hivi (jinsi kitu kinachozungumziwa kilivyo)

(d) (i) sawasa`wa (kwa kulingana, suluhu)
(ii) sawa`sawa (sio na hitilafu)

Mifano namba 4 (a-d) hapo juu inadhihirisha kuwa katika Kiswahili sanifu pale mkazo msingi unapohama kutoka katika silabi moja kwenda silabi nyingine husababisha maana ya msingi ya neno kubadilika.

**3.2 Uamilifu wa Mkazo katika Kiwango cha Tungo**
Uamilifu wa mkazo katika Kiswahili sanifu huweza kujitokeza pia katika kiwango cha tungo, kwa mfano katika tungo sentensi. Mgullu (1999:79) anaeleza kuwa wanaisimu wanaamini kwamba mkazo katika kiwango cha sentensi neno ambalo hukaziwa zaidi katika sentensi huelekea kuwa na umuhimu zaidi kuliko maneno mengine, hivyo katika maelezo yake anabainisha kuwa mkazo huweza kutumika pale mtu anapoulizwa swali na kuhitaji kujibiwa. Maelezo haya bado hayaelezi kwa uwazi uamilifu wa mkazo. Maelezo ya Mgullu (1999) yanaonesha kuwa anachanganya dhana ya mkazo na kiimbo. Kiimbo ni dhana ambayo huangalia dhima mbalimbali za tungo kama vile swali, ombi na taarifa. Hivyo, kutokana na mkanganyiko huu wa dhana ya kiimbo na mkazo makala hii inasaidia kutofautisha dhana hizo kuwa ni vipambasauti vyenye uamilifu tofauti. Hivyo, katika Kiswahili sanifu mkazo katika tungo una uamilifu ufuatao: Kwanza, hutofautisha neno lenye msikiko mkubwa zaidi kuliko msikiko wa maneno mengine katika tungo hiyo. Kama mfano wa 5 (a - b) unavyoonyesha hapo chini:

5 (a) Juma anakwenda soko`ni.
(b) Mwanafunzi hulipa a`da.

Mifano namba 5 (a - b) inaonesha waziwazi kabisa kuwa mkazo hutofautisha neno lenye msikiko mkubwa zaidi kuliko maneno mengine katika tungo inayohusika. Katika tungo 5(a) neno linalosikika kwa nguvu zaidi ni "*sokoni*" kuliko maneno mengine katika tungo hiyo. Pia katika tungo 5(b) neno linalosikika kwa nguvu zaidi ni "*ada*" kuliko maneno mengine katika tungo hiyo. Japokuwa maneno mengine katika tungo hizo yana mkazo lakini mkazo huo sio mkazo msingi ambao husikika kwa nguvu zaidi na kuweza kutofautisha nguvu ya msikiko kati ya vipandesauti vingine katika sentensi. Aidha unaweza kuwa mkazo upili au utatu yaani msikiko wake katika mkazo upili huwa na nguvu kiasi lakini mkazo utatu msikiko wake ni hafifu zaidi.

Pili, mkazo huonesha msisitizo wa jambo fulani. Msisitizo huu hutokana na mtindo unaoweza kujitokeza miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Hutokea pale ambapo mzungumzaji anaweka mkazo zaidi katika neno ambalo anataka kuweka msisitizo zaidi. Katika lugha ya Kiswahili mtindo huu hujitokeza hasa pale mzungumzaji anapoweka msisitizo kwenye neno la kwanza. Hali hii husababisha mkazo msingi kuhama kutoka katika nafasi yake ya neno la mwisho katika tungo na kuhamia kwenye neno la kwanza. Hebu tuone mfano wa 6 (a - b) hapo chini:

6 (a) (i) Juma anakwenda soko`ni. (Mazungumzo ya kawaida)
(ii) Ju`ma anakwenda sokoni. (Mazungumzo yenye kusisitiza kuwa Juma ndiye anayeenda sokoni)

(b) (i) Mwanafunzi hulipa a`da. (Mazungumzo ya kawaida)
(ii) Mwanafu`nzi hulipa ada. (Mazungumzo yenye kusisitiza kuwa mwanafunzi ndiye anayelipa ada).

Mifano iliyopo katika namba 6 (a - b) inaonesha wazi kuwa mkazo msingi unapohama kutoka neno la mwisho na kuhamia neno la kwanza huonesha msisitizo katika tungo hiyo. Kwa ujumla, uamilifu unaojibainisha katika kipambasauti mkazo katika kiwango cha tungo neno na tungo kirai katika Kiswahili sanifu unadhihirisha madai ya msingi ya kinadharia kuhusu mkazo kama yalivyoelezwa na Liberman na Prince (1977), Massamba (2011) na Hogg na McCully (1987).

**4. 0 Namna Mkazo Unavyotofautiana na Kiimbo na Kidatu**

Uamilifu wa mkazo unatusaidia kutofautisha kipambasauti mkazo na vipambasauti vingine kama vile kiimbo na kidatu katika Kiswahili sanifu. Kama tulivyoeleza kuwa mkazo katika Kiswahili sanifu hujitokeza pale ambapo silabi au neno hutamkwa kwa nguvu zaidi kuliko silabi au maneno mengine. Hali hii husababisha mkazo kuonesha msigano wa msikiko baina ya silabi au maneno katika viambajengo vinavyohusika. Pia mkazo huweza kuonesha msisitizo katika neno au tungo. Hali kadhalika, mkazo mara chache sana huweza kubadili maana ya msingi ya neno. Kwa upande wa kiimbo, ni kupanda na kushuka kwa sauti wakati wa usemaji, uimbaji au utoaji wa ukelele wa aina yoyote ile. Upandaji na ushukaji huo wa sauti hudhibitiwa zaidi na hali iliyokusudiwa na msemaji kama vile kutoa maelezo, kuuliza swali, kauli ya kejeli, kauli ya dharau na kadhalika (taz. Massamba, 2012: 159). Aidha, kidatu huhusu kiwango cha hali ya msikiko wa sauti kuwa ama juu, kati au chini (taz. Massamba, 2012: 161). Kiwango hiki cha sauti hakihusiani kabisa na ama uulizaji wa maswali, utoaji wa maelezo au kauli ya kejeli. Kutokuhusiana huko ni kwa sababu kauli zote hizo tunaweza kuzitumia katika kiwango chochote cha sauti yaani juu, kati au chini. Kwa mfano kiimbo katika kauli ya maelezo kinajidhihirisha katika mfano namba 7 (a-c) kama unavyoonekana hapo chini:

7 (a) amekwenda shule

•                    Kiwango cha juu

(b) amekwenda shule

•                    Kiwango cha kati

(c) amekwenda shule

•                    Kiwango cha chini

Mifano iliyopo katika namba 7 (a-c) inaonesha dhahiri kuwa kiimbo ni kilekile cha maelezo lakini kuna viwango mbalimbali vya kidatu, yaani kiwango cha juu, kati na chini. Hivyo inadhihirisha dhana ya kidatu katika kiimbo. Pia inaonekana wazi kabisa kuwa licha ya kiimbo na kidatu kujibainisha katika data hiyo lakini haijaathiri uamilifu wa mkazo katika tungo hiyo. Yaani katika tungo "*amekwenda sokoni*" neno "*sokoni*" linasikika kwa nguvu zaidi kwa sababu limebeba mkazo msingi lakini neno "*amekwenda*" lina msikiko hafifu zaidi kuliko neno "*sokoni*".

Hata hivyo, baada ya kuona tofauti hizo zinavyojibainisha kati ya mkazo, kiimbo na kidatu, kuna wakati mkazo unaweza kuathiriwa na kiimbo au kidatu. Kwa mfano, katika kiimbo cha kuuliza swali husababisha kuathiri mkazo, yaani kiwango cha msikiko wa sauti katika kiambajengo kinachohusika husikika kwa nguvu zaidi. Haya yanadhihirishwa katika mfano namba 8 hapo chini:

8. "amekwenda shule?"

•

Mfano namba 8 unaonesha dhahiri kuwa tungo hiyo kwa sababu ya kiimbo cha kuuliza swali kimesababisha mkazo katika neno "*shule*" kuongezeka nguvu zaidi kimsikiko. Hali hii ni tofauti na kiwango cha msikiko katika neno "*shule*" kwenye mfano namba 7 (a-c). Hata hivyo, licha ya athari hiyo ya kimsikiko, bado mkazo msingi upo katika neno hilo "*shule*" yaani linasikika zaidi kuliko neno "*anakwenda*" katika tungo hiyo.

**5.0 Hitimisho**

Makala hii imesaidia kuonesha uamilifu wa mkazo katika Kiswahili sanifu. Uamilifu wa mkazo ni muhimu kuubainisha kwa sababu unasaidia kukamilisha uzungumzaji katika utamkaji wa viambajengo vinavyohusika. Pia unasaidia kutofautisha mkazo na vipambasauti vingine katika Kiswahili sanifu. Hivyo, uamilifu wa mkazo ni tofauti na uamilifu wa kiimbo na kidatu katika Kiswahili sanifu. Hata hivyo, kutokana na ujibainishaji wa kipambasauti mkazo katika Kiswahili sanifu, kuna haja ya kufanya uchunguzi wa kina ili kuweza kubaini ruwaza ya mkazo katika Kiswahili sanifu.

## Marejeleo


Chomsky, N. na M. Halle (1968). *Sound Parten of English.* New York: Harper and Row.

Crystal, D. (1987). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*. Toleo la 2: U. S. A: Basil Blackwell Ltd.

Halle, M. na G. N Clements (1983). *Problem Book in Phonology. A Workbook for Introductory Courses in Linguistics and in Modern Phonology*. London: The MIT Press.

Halle, M. na J-R. Vergnaud (1978). *Metrical Structures in Phonology*. Cambridge, MA: MIT Press.

Harrington, J. na Cox, F. (2009). *Phonetics and Phonology (The Foot and Word Stress).* http://class.mq.edu.au/speech/phonetics/phonology stress. Jumamosi, 15 Aprili, 2016.

Hogg, R. McCully, C. B. (1987). *Metrical Phonology: A Coursebook.* Cambridge: Cambridge University Press.

Kager, R. (1996). "The Metrical Theory of Word Stress". Katika Goldsmith, J. A. (mh.) *The Handbook of Phonology Theory.* Cambridge, Massachusetts: Blackwell Publishers Ltd.

Kihore, Y. M, D. P. B. Massamba na Y. P. Msanjila (2008). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo*. Chapa ya Nne, Dar es Salaam: TUKI.

Liberman, M. (1975). *The Intonation System of English. PhD dissertation MIT.* Bloomington: Indiana University Linguistics Club.

Liberman, M. na A. Prince (1977). "On Stress and Linguistics Rhythm". Katika Linguistics Inquiry 8: 249-336.

Massamba, D. P. B (2002). *Historia ya Kiswahili: 50 BK hadi 1500 BK*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

______(2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TATAKI.

_____ (2012). *Misingi ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TATAKI.

Massamba, D. P. B., Y. M Kihore na Y. P. Msanjila (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, S. R (1999). *Mtaala wa Isimu*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.